Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Majadiliano Juu Ya Ufumbuzi

1. Wakati tunapoomba kwa Allah (s.w.t.) kuwaachilia wafungwa wote, hatuombi kuachiliwa kwa kila aina ya mfungwa, awe mfungwa wa Allah au mfungwa wa Shetani. Bali tunaomba kwa ajili ya wale wafungwa wote ambao ufungwa wao huwazuia kutokana na ufanisi wa kimwili na kiroho. Hata hivyo, wokovu kutokana na ufungwa wa kiroho kama tulivyotaja hapo juu, uko mikononi mwa mfungwa mwenyewe. Kama akiamka kutoka kwenye usingizi wake mzito na kubadilisha tabia zake mbovu, atajipa uhuru yeye mwenyewe. Na ambaye anafanikiwa katika kufanya hivyo, anaweza kujitahidi kueneza utamaduni wa jinsi ya kuwapa huru watu wengine kutoka kwenye minyororo ya ufungwa wa kiroho, na hatimaye kutafsiri kifungu hiki chenye nuru cha maombi kwenye vitendo.

2. Wakati mwingine ufungwa wote, wa kimwili na wa kiroho ni wa haki, na makosa ya mfungwa mwenyewe, kwa mfano: kama mtu kwa makusudi angeiba au akapendelea matamanio ya kiduniya kuliko sheria ya Mwenyezi Mungu. Hivyo, muombaji lazima vile vile ajaribu kwa unyenyekevu kuomba kuondolewa sababu ambazo humpelekea kwenye ufungwa huo. Kwa kweli aina zote za ufungwa katika hali ya usawa wake huanzia kwenye *ittibaa' al- hawa* (kufuata mielekeo miovu). Kwa hiyo, lazima tuombe kwamba, utamaduni wa *taqwa* unapenyeza kwenye jamii zetu ili kwamba 'ufungwa' wa kweli unatoweka.

3. Matukio mengi ya ufungwa katika nyakati zote ni udhihirisho wa uonevu wa serikali za kitaghuti. Vitendo kama hivyo vinaweza kuondolewa kwa umoja wa umma kuziasi serikali zao. Kama umma ukiendeleza upinzani huo, kwa hakika utaitishia serikali, na kutakuwa na nafasi ya kuachiwa wafungwa wasio na hatia.

4. Idadi imara ya dola zijiitazo za ki-Islamu zinaweza kuzuiya uuwaji wa halaiki wa mataifa makubwa yenye kiu ya damu, kwani moja ya vyanzo muhimu sana vya nishati viko mikononi mwao; mafuta, au 'dhahabu nyeusi.' Suala la Palestina vile vile linaweza kutatuliwa kwa urahisi sana na wao. Lakini ni maslahi ya maovu ndio ambayo yanawazuia kutumia akili zao, na katika mlolongo huo unawafanya wapate fedheha ya milele ya kiroho.

Source URL: https://www.al-islam.org/fr/node/39638#comment-0